TANGAZO LA SERIKALI NA. 698 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA IGAGALA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Igagala ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka I1 iliyopo katika kona ya barabara ya Kigoma katika majira-nukta 362551E, 9451025N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki-Kaskazini katika uelekeo E170$^0$11'20"N kwa umbali wa kilomita 2.2 hadi alama ya mpaka I2 yenye majira-nukta 364731E, 9451344N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata barabara ya Kigoma na uelekeo wa N93$^0$6'12" kwa umbali wa kilomita 3.1 hadi alama ya mpaka I3 iliyopo katika mto wa msimu wa Igagala Na. 9 yenye majira-nukta 364734E, 9454444N; baada ya hapo mpaka unafuata uelekeo wa mto kuelekea Magharibi-Kusini na kupita barabara ya Kigoma katika alama ya mpaka I4 yenye majira-nukta 362428E, 9453699N; baada ya hapo mpaka unaendelea kufuata uelekeo wa mto Magharibi-Kusini hadi alama ya mpaka I5 yenye majira-nukta 360671E, 9453512N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa S98$^0$6'32" kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi alama ya mpaka I6 yenye majira-nukta 360792E, 9451260N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki-Kusini katika uelekeo wa E94$^0$6'16" kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*